

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR**

08/07/2024

**TAARIFA KWA UMMA JUU YA BEI ZA MAFUTA KWA MWEZI JULAI 2024.**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) inatangaza Bei za Mafuta kwa Mwezi Julai, 2024 zitakazoanza kutumika rasmi kuanzia Siku ya Jumanne, Tarehe, 09/07/2024.

Mamlaka hupanga bei kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta Duniani (Platts Quatations).
- Gharama za uingizaji Mafuta katika bandari ya Dar-es-Salaam na Tanga.
- Gharama za mabadiliko ya Fedha za kigeni zinazotumika kununulia Mafuta.
- Gharama za Usafiri, Bima na 'Premium' hadi Zanzibar.
- Kodi na Tozo za Serikali.
- Kiwango cha faida kwa Wauzaji wa Jumla na Reja Reja.

Bei za mafuta kwa Mwezi Julai, 2024 ni kama zifuatazo:

| AINA YA MAFUTA  | BEI YA MWEZI JUNE, 2024 (TZS/LITA) | BEI YA MWEZI JULAI, 2024 (TZS/LITA) | TOFAUTI (TZS/LITA) | TOFAUTI ASILIMIA |
|-----------------|------------------------------------|-------------------------------------|--------------------|------------------|
| PETROLI         | 3,132                              | 3,085                               | -47                | -1.50            |
| DIZELI          | 3,068                              | 3,074                               | 6                  | 0.55             |
| MAFUTA YA TAA   | 3,200                              | 3,200                               | 0                  | 0.00             |
| MAFUTA YA NDEGE | 2,877                              | 2,809                               | -68                | -2.36            |

Sababu, za kupungua kwa Bei ya Petroli na Mafuta ya Ndege ni kupungua kwa gharama za Mafuta katika Soko la Dunia na kupungua kwa gharama za uingizaji wa mafuta pamoja na mabadiliko ya Fedha za Kigeni, na sababu za kuongezeka kwa Bei ya Dizeli ni kuongezeka kwa gharama za Mafuta katika Soko la Dunia.

Aidha, Mamlaka inawahimiza Wananchi kununua Mafuta katika Vituo halali vya Mafuta na kudai Risiti za Kielektroniki kila wanaponunua Mafuta.

**IMETOLEWA NA KITENGO CHA UHUSIANO (ZURA)**

